

**KUOMBEA WATU NA MAZINGIRA
YA GIZANI**



NURU KATIKA GIZA:

“Na kuwe mwanga”

Yesu anamuhimiza mtakafu Paulo na sisi kutenda katika roho ya msamaria mwema (luka 10:29-37)

“Nawatuma ninyi kwao mkawafumbue macho yao na kuwageuza kutoka gizani kuingla mwangani; na kutoka kwa nguvu za shetani na kumgeukia Mungu, ili wapate msamaha wa dhambi na mahali kati ya waliotakasika kwa njia ya Imani ndani yangu.” (matendo ya mitume 26:18)

Yesu anatuita kuwasaidia wanaoteseka.

Anasema,

“chochote muntendeacho mdogo wa hawa mwanitendea mimi.” Mt. 25:40

Tunawaalika mjiunge na jumua yetu ya sala katika mwito wetu wa kuwa wasamaria wema, Kwa kuwaombea walionaswa katika giza kuu; na kuomba kwa nia maalum ya kumsihi Mungu aweke huru, Watu na mikakati ya kijamii iliyosongwa na uovu.

Basi tunawasihi mjiunge nasi kwa dakika chache kila siku, kuwaombea walioathiriwa na wahalifu. Umuombe Mungu kupitia kwa huruma takatifu ya Yesu aguse mioyo yao, awageuze kwa maadili ya injili na kuponya majeraha yao.

Imani yetu ya msingi ni kuwa: Uovu uko na unafanya kazi duniani. Sala zaweza kuvunja ufungwa wa shetani. Sala huamsha roho mtakatifu ndani ya walio gizani. Nguvu ya sala yabadilisha mambo. Sala ni jawabu ya amri kuu kupendana. Wote wawili muombaji na mwenye kuombewa hubadilika. Tumetumwa na kristu kama wasamaria wema kuleta nuru gizani kwa njia ya sala.

Mifano michache ya gizani:

Vita vya kijamii na makundi ya kilevi; Ulevi na usafirishaji wa madawa ya kulevya; Mazoea mengine mabaya sana; Matumizi na uenezaji wa picha za kipunografia (mambo ya Ngoni); Biashara zinazohusisha utumwa wa kibinadamu, Ukahaba; Tabia ya kibaguzi na uoga uliofichika; Utoaji mimba na uuaji kwa madai ya huruma Massengenyo yenye uovu uliojificha; Mikakati ya kiuchumi isiyo haki inayochangia umaskini na unyanyasaji wa binadamu; Na kuendeleza mapigano, ugaidi na uuaji; Mizungu na Vitendo vya kishetani; Upweke na Sonono; Majivuno, Hasira, Mizungu na Tamaa, Hofu na Kutosamehe.

Tuombe:

Twawainua mbele zako Bwana Yesu, wale wote waliofungwa na aina yoyote ya maovu. Huruma yako idhihirike hata palipo na giza kuu na dhambi.

Kwa nguvu na kifo chako na ufufuko wako ee Yesu, ulishinda uovu na kufungua milango ya uadilifu na utakatifu. Ushiriki wako dhidi ya uovu na kifo ulete uponyaji, uzima na matumaini mioyoni kote ulimwenguni.

Kwa njia ya kipekee, nainua

(taja watu/hali)

Twaomba haya kwa jina la Bwana na Mkombozi wetu, Yesu Kristo. Amina.

Please find us @ www.litdplus.com/facebook

Ecclesiastical Approval Granted by Msgr. John P. Zenz, V.G.

Archdiocese of Detroit May 23, 2008

Please feel free to duplicate or reorder at
aodprintshop 313-237-5967